# Sherehe ya Harusi (Wedding Ceremony)

[Jina la Bwana harusi] na [Jina la Bibi harusi], pamoja na familia zao na marafiki zao, wanatambua uwepo wenu ili kushiriki furaha na kushuhudia patano lao pamoja.

Baada ya kupendana mmoja na mwingine, [Jina la kwanza la Bwana harusi ] na [Jina la kwanza la Bibi harusi ] wameamua kutoa maisha yao mmoja kwa mwingine na kwa hivyo leo wataungwanishwa kama mume na mke.

Kama itapendeza: Ombi linaweza tolewa au somo la Biblia na mmoja wa mwanafamilia au hata rafiki yao.

**Mchungaji awaambie wanao oana :**

Ndoa ni muungano wa asili kati ya mume na mke, mmungano takatifu, ulioanzishwa na Mwenyezi Mungu. Hapo mwanzo, Mungu alitoa mwelekeo wa ndoa kwa kuwaunganisha Adamu na Hawa.

Mungu alipoumba uhai katika ulimwengu, aliwaumba wanadamu katika mfano wake, wawe na uwezo wa kuwa na uhusiano naye na wao kwa wao. Akawapa wanadamu akili ya kuwa wabunifu, kufanya maamuzi, kuunda mipangilio na kuendesha maisha yao kulingana na mipangilio walioweka. Kama Baba mpendwa, Mungu alitupatia ushirika wa ndoa na Baraka ya familia ili tuweze kushiriki katika neema na upendo wake kwetu.

Mungu alimuumba hawa kutoka kwenye nyama na mifupa ya Adamu na akawaunganisha kama mume na mke “Kwa hiyo mwanamume atawacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.”[1] “Mungu akawabariki, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha;[2]

Kwa kuwa ndoa ni takatifu, na mwanzilishi wake ni Mungu wakati wa uumbaji na ikasisitizwa na Bwana wetu Yesu Kristo, sio suala la kujiingiza kimzaha, lakini kwa umakini na kwa furaha mbele zake Mungu.

Utamanduni wetu unaweza kuwa na desturi zake na sheria zinazosimamia ndoa, lakini katika kanisa ndoa inaundwa kwa kutegemea msingi na mamlaka ya Mungu kama inavyofunuliwa katika maandiko. Ndoa sio muungano wa kimwili tu bali ni muungano wa kiroho pia.

Yesu alisema, “Lakini tangu mwanzo wa kuumbwa ulimwengu, aliwafanya mume na mke. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambataba ba mkewe, na hao wawili watakuwa mwili mmoja; hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe.[3]

---

[1] Mwanzo 2:24 , Nukuu zote kutoka kwenye NIV tafsiri ya 2011
[2] Mwanzo 1:28.
[3] Marko 10:6-10

Mtume Paulo aliandika kuhusu ndoa:

> Hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo. Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo.
>
> Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa. Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe.[4]

Ndoa ni muungano mtakatifu, uhusiano wenye dhamana unaostawi katika mazingira ya kuhurumiana, kujitoa na kuhudumiana. Ndoa inatokana na mapenzi na ni kwa sababu ya mapenzi na misingi yake ni mapenzi.

Mtume Paulo anatukumbusha uhusiano wetu unatakiwa kuwa wa unyenyekevu na kuheshimiana sio tu kwenye ndoa bali kwa mahusiano yetu yote, lakini inatakiwa zaidi katika maisha ya ndoa.

> Basi ikiwako faraja yo yote katika Kristo, yakiwako matulizo yo yote ya mapenzi, ukiwako ushirika wo wote war oho, ikiwako huruma yo yote na rehema, ijalizeni furaha yangu, ili mwe na nia moja, wenye mapenzi mamoja, wenye roho moja, mkinia mamoja. Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo yaw engine. Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwemo pia ndani ya Kristo Yesu;[5]

Mapatano ya ndoa mtakayopatana hapa leo yanawataka kila mmoja ajitoe kwa mwenzake kumuenzi, kutukuza na, kumheshimu wenzako, kila wakati kutoa nafasi kwa manufaa ya mwenzako kwa upendo na kujitoa. Ni kushiriki kwako kwa mwingine ndani ya upendo wa Mungu ndiko kutaimalisha na kuilinda ndoa yako.

Mchungaji anaweza kusoma 1 Wakorintho 13:4-8:

> Upendo huvumilia, upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote. Upendo haupungui neno wakati wo wote;

[4] Waefeso 5:21-28.
[5] Wafilipi 2:1-5.

> bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika.[6]

Kama Baba mpendwo, Mungu anapenda upate Baraka za kipekee na furaha. Kwa hali hiyo amewapa (majina ya wanaooana), kila mmoja kwa mwingine kwa Baraka ya kipekee.

Yesu alisema "Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma". (Yohana 17:3).

Mnavyoendelea kufahamiana zaidi katika miaka inayokuja, ni vema uhusiano wenu katika muungano huu mtakatifu uendelee kujengwa kwa kuwaza neema na upendo wa Mungu usio wa masharti na usio isha.

Upendo huu kila mara ukutangulie. Mshikamane na muwe karibu kwa kutimiziana nathiri mlizowekeana hapa leo, ili muweze mbele ya Kristo na msaada wake muanzishe familia ambayo haitatizwa na mawimbi wala mabandiliko na changamoto za maisha.

**Nadhiri:**

Je, kwa hali hiyo, [Majina yote ya mwanaume], kwa uaminifu ahidi, kwa mapatano mbele za Mungu na mbele za mashahidi hawa, kuchukua [Majina yote ya mwanamke] awe mke wako, uliyemuoa kisheria, kwa maisha ya uhai wenu, kumpenda, kumuenzi, kumheshimu, kumtunza na kumgharamikia?

Mwanaume anaahidi "Ndio naahidi"

Na wewe, [Majina yote ya mwanamke], kwa uaminifu ahidi, kwa mapatano mbele za Mungu na mbele za mashahidi hawa, kuchukua [Majina yote ya mwanaume], awe mume wako, uliyekuoa kisheria, kwa maisha ya uhai wenu, kumpenda, kumuenzi, kumfariji na kumheshimu?

Mwanamke anaahidi "Ndio naahidi"

[Mwanaume na Mwanamke wanageuka na kutazamana huku wakishikana mikono]

Mchungaji anasema Minister says: "[Jina la kwanza la Bwana harusi ], tafadhali rudia baada yangu":

> Mimi, [Majina yote ya mwanaume], kwa msaada wa mwenyezi Mungu, nakuchukua wewe [Majina yote ya mwanamke] kuwa mke wangu halali wa ndoa, kuwa nawe, kukushikilia, kutoka siku ya leo na kuendelea, wakati wa hali nzuri na wa shida, wakati wa raha na dhiki, wakati wa afya njema na wakati wa

[6] 1 Wakorintho 13:4-8, New Living Translation.

> magonjwa, ili kupenda na kuenzi mpaka kifo kitakapotutenganisha. Hili ninaahidi kwako.

Mchungaji sasa asema: "[Jina la kwanza la Bibi harusi ], tafadhali rudia baada yangu":

> Mimi, [Majina yote ya mwanamke], kwa msaada wa mwenyezi Mungu, nakuchukua wewe [Majina yote ya mwanamume] kuwa mume wangu halali wa ndoa, kuwa nawe, kukushikilia, kutoka siku ya leo na kuendelea, wakati wa hali nzuri na wa shida, wakati wa raha na dhiki, wakati wa afya njema na wakati wa magonjwa, ili kupenda na kuenzi mpaka kifo kitakapotutenganisha. Hili ninaahidi kwako.

Tafadhali shikaneni mikono tunapomshukuru Mungu kwa Baraka ya ndoa yenu.

Wanaweza kupiga magoti (Haya ni maamuzi yao).

Mchungaji aongoze kwa maombi ya shukrani.

Mchungaji sasa asema: "Sasa mnaweza kuvishana pete, ambazo ni ishara ya nje tu kuonyesha upendo wenu, kujitoa na mshikamano kati yenu"

Wana ndoa wanavishana pete.

Mchungaji sasa asema: "Kwa mamlaka ya Yesu Kristo na [Jina la Serikali ya mtaa], Sasa nawatangaza kuwa mume na mke. Unaweza kumbusu mke wako"

Mchungaji anawaambia waliohudhuria: "Nawakabidhi [Bwana na Bibi-Majina kama walivyochagua walioana]